

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU SAYANSI TEKNOLOJIA

NA UFUNDI



MTAALA WA ELIMUMSINGI

DARASA LA I NA LA II

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU SAYANSI TEKNOLOJIA

NA UFUNDI

MTAALA WA ELIMUMSINGI

DARASA LA I NA LA II

2015

© Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, 2015

Toleo la Kwanza, 2015

Toleo la Pili, 2016

ISBN.978 9976 61 394 0

Taasisi ya Elimu Tanzania

S.L.P 35094

Dar es Salaam.

Simu:+255 22 2773005/+255 22 277 1358

Faksi: +255 22 2774420

Tovuti:www.tie.go.tz

Baruapepe: director.general@tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa au kutoa andiko hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Kamishna wa Elimu, Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi.

Yaliyomo

Majedwali.....	iv
Vifupisho.....	v
Ujumbe kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.....	vi
Dibaji	vii
1.0 UTANGULIZI.....	1
1.1 Usuli.....	1
1.2 Sababu za Kubadili Mtaala wa Shule za Msingi kwa Darasa la I na la II.....	1
1.3 Muktadha wa Mtaala.....	2
1.4 Malengo ya Mtaala.....	2
2.0 Muundo wa Mtaala na Maudhui.....	2
2.1 Umahiri katika Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.....	3
2.2 Umahiri katika Stadi Wezeshi.....	4
3.0 Muda wa Kufundisha na Idadi ya Vipindi.....	4
4.0 Viwango vya Rasilimali katika Utekelezaji wa Mtaala.....	5
4.1 Rasilimali watu: Mwalimu mahiri wa KKK.....	5
4.2 Rasilimali Vitu.....	6
4.2.1 Sifa za Mazingira ya Ujifunzaji na Ufundishaji wa KKK.....	6
4.2.2 Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia.....	7
5.0 Ujifunzaji na Ufundishaji.....	7
6.0 Usimamizi.....	8
7.0 Ufutiliaji na Tathmini.....	8
8.0 Upimaji wa Ujifunzaji.....	9
8.1 Upimaji wa Awali.....	9
8.2 Upimaji Gunduzi na Majaribio Chekeche.....	9
8.3 Upimaji Endelesi.....	9
8.4 Upimaji wa Kitaifa.....	9
9.0 Matokeo ya Ujifunzaji na Viwango vya Upimaji.....	10
9.1 Upimaji wa Shughuli/kazi za Kusoma.....	10
9.2 Upimaji wa Shughuli/ kazi za Kuandika.....	10
9.3 Upimaji wa Shughuli/kazi za Kuhesabu.....	11

Majedwali

Jedwali 1: Umahiri katika KKK Darasa la I	3
Jedwali 2: Umahiri katika KKK Darasa la II	3
Jedwali 3: Umahiri katika stadi wezeshi	4
Jedwali 4: Mgawanyo wa muda wa kufundisha vipindi	5
Jedwali 5: Vigezo vya upimaji na utendaji	10

Vifupisho

CBP	Childrens' Book Project
EQUIP -T	Education Quality Improvement Program in Tanzania
GPE	Global Partnership for Education
KKK	Kusoma, Kuandika na Kuhesabu
LANES	Literacy and Numeracy Education Support
MKUKUTA	Mpango wa Taifa wa Kuinua Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania
MMEM	Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi
NECTA	National Examination Council of Tanzania
OR-TAMISEMI	Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
TEHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
TET	Taasisi ya Elimu Tanzania
TZ21	Tanzania 21 st Century Basic Education Program
UNESCO	United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization
USAID	United States Agency for Internaional Development
WESTU	Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundı

Ujumbe kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania

Mtaala wa Elimumsingi Darasa la I na la II ambao umeweka mkazo katika stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu umelenga kuboresha toleo la mtaala wa darasa la I na la II mwaka 2015. Toleo hili la pili limeboreshwa katika maeneo ya upimaji, ufuatiliaji na tathmini pamoja na eneo la matokeo ya ujifunzaji na viwango vya upimaji. Ni matumaini yangu kuwa mtaala huu utazidi kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK katika shule zetu. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatoa shukurani kwa wadau wote walioshiriki katika kuboresha mtaala huu na viongozi waliosimamia kazi kwa ufanisi.



Dkt. Elia Y. Kibga
Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Taasisi ya Elimu Tanzania

Dibaji

Uamuzi wa kuboresha Mtaala wa Darasa la I na la II unatokana na malengo ya Serikali ya kukuza stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). Mtaala umeandalowiwa kwa kuzingatia viunzi na miongozo mbalimbali kuhusu ujifunzaji wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu kwa wanafunzi wa Darasa la I na la II. Pia umezingatia mtaala wa mwaka 2005, kwa lengo la kutambua maeneo mengine muhimu ya kujifunza kwa wanafunzi wa Darasa la 1 na la II. Mtaala unazingatia kwamba miaka ya mwanzo ya kujifunza ni muhimu sana katika makuzi ya mtoto kiakili, kimwili na kijamii.

Stadi za KKK ni msingi muhimu katika kumwezesha mwanafunzi kujifunza kwa ufanisi na kumudu masomo yake katika ngazi za juu kwa ubora unaotakiwa. Mtaala huu unalenga katika kumjengea mwanafunzi stadi za KKK kupitia shughuli/kazi mbalimbali atakazozifanya wakati wa mchakato wa kujifunza. Hivyo basi, kazi kubwa ya mwalimu ni kumwezesha mwanafunzi kujifunza na kumudu stadi za KKK.

Mtaala huu umetafsiriwa katika miongozo mbalimbali ili kuwawezesha watumiaji kuutekeleza kama ilivyokusudiwa. Mwongozo mkuu wa utekelezaji wa mtaala ni muhtasari ambaao utatumia na mwalimu wakati wa ufundishaji. Hata hivyo; mwalimu anatakiwa kupitia mtaala huu ili aweze kuwa na mtazamo mpana kuhusu kile anachotekeleza. Ni muhimu pia kwa wadau wengine wa elimu kutumia mtaala huu katika kutekeleza na kufuatilia ujifunzaji wa stadi za KKK kwa wanafunzi wa Darasa la I na la II. Mtaala huu utaendelea kupitiwa na kuboreshwa hivyo maoni yoyote yapelekwe kwa Mkurugenzi Mkuu, Taasisi ya Elimu Tanzania.



Prof. Eustella Bhalalusesa
Kamishna wa Elimu
Wizara ya Elimu Sayansi Teknolojia na Ufundi

1.0 UTANGULIZI

1.1 Usuli

Mtaala wa Elimu ya Msingi ulirekebishwa mwaka 2005 ili kukidhi mahitaji ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, Mpango wa kisekta wa Maendeleo ya Elimu wa 1999 – 2009 na Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025. Pia marekebisho yalizingatia Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MMEM) 2000-2006, Mpango wa Taifa wa Kuinua Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) na mapendekezo ya tafiti anuai za kielimu na maoni ya wadau wa elimu. Aidha, marekebisho hayo yalizingatia mahitaji ya jamii, sayansi na teknolojia pamoja na mtazamo wa ufundishaji na ujifunzaji ambao unamlenga wanafunzi.

Katika ufuataliaji wa utekelezaji wa mtaala wa mwaka 2005, ilibainika kwamba kuna wanafunzi wenye matatizo katika stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). Stadi hizi ni za msingi na muhimu katika kumwezesha wanafunzi kujifunza kwa ufanisi na kumudu masomo yake katika ngazi za juu kwa ubora unaotakiwa. Hivyo mwaka 2013 ulifanyika utafiti wa kitaifa wa kupima uwezo wa wanafunzi wa Darasa la II katika stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Lengo la upimaji huo lilikuwa ni kubaini kiwango cha wanafunzi katika umahiri wa stadi hizo za msingi. Matokeo ya utafiti huo yalionesha kwamba kuna tatizo kubwa la wanafunzi kutokuwa na umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Hivyo, serikali imeona umuhimu wa kuandaa mtaala kwa Darasa la I na la II ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanajifunza kikamilifu na kujenga stadi hizo.

Mtaala huu una Utangulizi, Muundo wa Mtaala na Maudhui, Muda wa Kufundisha na Idadi ya Vipindi, Viwango vya Rasilimali katika Utekelezaji wa Mtaala, Ujifunzaji na Ufundishaji, Usimamizi, Ufuataliaji na Tathmini, Matokeo ya Ujifunzaji na Viwango vya Upimaji.

1.2 Sababu za kubadili Mtaala wa Shule za Msingi kwa Darasa la I na II

Mtaala wa Elimu ya Msingi wa mwaka 2005, ulijumuisha Darasa la 1 hadi la VII. Tafiti zinaonesha kwamba, mtaala huo kwa Darasa la I na la II ulikuwa umesheheneza masomo na hivyo kuwafanya walimu kufundisha maudhui ya masomo kuliko stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Masomo yaliyokuwepo kwenye mtaala huo ni Kiswahili, Hisabati, English, Sayansi, Stadi za Kazi, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Haiba na Michezo.

Katika kukuza uwezo wa wanafunzi wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu kumekuwa na haja ya kuwa na mtaala wa pekee kwa Darasa la I na la II. Mtaala huu umeandaliwa kwa kuzingatia mahitaji kutoka kwa wadau mbalimbali kama wazazi, walimu, wanafunzi, wakufunzi, watafiti na wadau wengine ambao walitoa ushauri unaofanana. Mtaala huu unajikita zaidi katika kuimarisha umahiri wa wanafunzi kwenye stadi za KKK na unachukua nafasi ya Mtaala wa mwaka 2005 kwa Darasa la I na la II.

1.3 Muktadha wa Mtaala

Mtaala huu wa Darasa la I na la II unaendana na muktadha wa kijamii, kiuchumi na kisiasa katika karne hii ya 21. Mtaala umezingatia kukua kwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ambayo ina mchango mkubwa katika kujifunza stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Kutokana na kuongezeka kwa ushirikiano baina ya watu na mataifa unaochangiwa na utandawazi, mtaala umetayarishwa kwa kuzingatia mahitaji ya Kitaifa na Kimataifa.

Tafiti zinaonesha kuwa mtoto hujifunza vizuri zaidi pale anapoanza kujifunza kwa lugha anayoifahamu. Pia humsaidia kuepusha mkanganyiko wa matamshi ya herufi ambao hujitokeza wakati wa kujifunza lugha mbili tofauti kwa wakati mmoja. Kwa upande mwingine tafiti zinaonesha kwamba mtoto akimudu vema lugha yake ya kwanza inamsaidia kujifunza kiurahisi lugha nyingine. Hivyo mtaala huu unasisitiza matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia ambayo ni ya Taifa na inazungumzwa na watanzania wengi.

1.4 Malengo ya Mtaala

Mtaala umeandalowiwa ili mwanafunzi aweze:

- i) Kukuza stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu;
- ii) Kuwasiliana kwa njia sahili;
- iii) Kutunza afya;
- iv) Kujenga uimara wa mwili na kushirikiana na wengine;
- v) Kuwa na mtazamo chanya kuhusu kujifunza;
- vi) Kuthamini mazingira;
- vii) Kujitambua na kukuza vipaji;
- viii) Kukua kimaadili;
- ix) Kukua kiimani kwa mujibu wa dini yake.

2.0 Muundo wa Mtaala na Maudhui

Mtaala huu umejikita katika umahiri na umegawanyika katika maeneo mawili makuu ya kujifunza ambayo ni stadi za KKK na Stadi Wezeshi. Stadi za KKK ndio eneo la msingi katika mtaala huu na linalenga kuwawezesha wanafunzi wa Darasa la I na la II Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Hata hivyo stadi hizi hujengwa pamoja na stadi za kusikiliza na kuzungumza. Eneo la Stadi Wezeshi linajikita katika stadi nyingine ambazo zikikuzwa zitamsaidia mwanafunzi kujifunza Kusoma, Kuandika na Kuhesabu na kukabiliana na maisha yake ya kila siku. Hivyo basi, katika mtaala huu stadi nyingine ni za kumjenga mwanafunzi kiafya, kimwili, kiakili na kisaikolojia kwa kushiriki katika michezo, kuchora, kuimba, kuigiza na elimu ya dini ambayo ina nafasi kubwa katika kumsaidia mwanafunzi kukua kiroho na kimaadili.

2.1 Umahiri katika Kusoma, Kuandika na Kuhesabu

Mtaala huu umejikita katika umahiri ambao utamwezesha mwanafunzi Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Jedwali la 1 na la 2 linaonesha uwezo wa kutenda ambao mwanafunzi anategemewa kuujengwa katika Darasa la I na la II.

Jedwali 1: Umahiri katika KKK Darasa la I

Namba	KUSOMA	KUANDIKA	KUHESABU
1	Lugha ya mazungumzo	Misingi ya kuandika	Utambuzi wa dhana ya namba
2.	Utambuzi wa sauti	Uumbaji wa herufi	Utambuzi wa uhusiano wa idadi ya vitu na namba
3.	Utambuzi wa sauti za herufi	Matumizi ya kanuni za uandishi	Matumizi ya matendo katika namba
4.	Matumizi ya msamiati	Ufasaha na ushikamani	Utambuzi wa maumbo
5.	Ufahamu wa Kusoma na Kusikiliza	Uandishi wenye mfuatano sahihi wa matukio	Utambuzi wa vipimo
6.	Kusoma kwa ufasaha	Uandishi wa mwandiko wa chapa	Kukusanya na kuorodhesha vitu

Jedwali 2: Umahiri katika KKK Darasa la II

Namba	KUSOMA	KUANDIKA	KUHESABU
1.	Lugha ya mazungumzo	Uumbaji wa herufi	Utambuzi wa dhana ya namba
2.	Utambuzi wa sauti	Uundaji wa maneno	Utambuzi wa uhusiano wa idadi ya vitu na namba
3.	Utambuzi wa sauti za herufi	Kuandika kwa mfuatano sahihi wa matukio	Matumizi ya matendo katika namba
4.	Matumizi ya msamiati	Matumizi ya kanuni za uandishi	Utambuzi wa maumbo
5.	Ufahamu wa kusoma na kusikiliza	Ufasaha na ushikamani	Utambuzi wa vipimo
6.	Kusoma kwa ufasaha		Kukusanya na kuorodhesha vitu

2.2 Umahiri katika Stadi Wezeshi

Eneo la stadi wezeshi limejikita katika umahiri kama ilivyo katika stadi za KKK. Jedwali la 3 linaonesha uwezo wa kutenda ambao mwanafunzi anategemewa kuujenga katika Darasa la I na la II.

Jedwali 3: Umahiri katika Stadi Wezeshi Darasa la 1 na la II

Namba	Umahiri katika Kutunza Afya na Mazingira	Umahiri katika Kuendeleza Michezo na Sanaa
1.	Kubaini njia za kujikinga na magonjwa	Kucheza michezo sahihi
2.	Kutambua sehemu za nje za mwili wa binadamu	Kuonesha mwenendo sahihi wa mwanamichezo
3.	Kutambua viumbe hai	Kutambua kanuni katika michezo na sanaa
4.	Kutoa huduma ya kwanza	Kuwasiliana kupitia sanaa
5.	Kusafisha na kutunza mazingira	Kubuni na kuimarisha stadi za michezo na sanaa.

3.0 Muda wa Kufundisha na Idadi ya Vipindi

Mwaka wa shule utakuwa na siku 194 ambao ni sawa na wiki 39. Mwaka umegawanywa katika mihula miwili, hivyo kutakuwa na mihula miwili (2) ya masomo. Kila muhula utakuwa na wiki mbili (2) zitakazotumika kwa upimaji. Ili kufikia malengo ya mtaala huu na kupata matokeo yanayotarajiwa, mwanafunzi wa Darasa la I na la II atasoma masomo sita (6) ambayo ni Kusoma, Kuandika, Kuhesabu, Kutunza Afya na Mazingira na Kuendeleza Michezo na Sanaa pamoja na Elimu ya Dini.

Muda wa kufundisha kwa wiki ni saa 15 na kutakuwa na vipindi sita (6) kwa siku. Kila kipindi kitatumia muda wa dakika 30 tu. Hivyo katika siku moja ya mafunzo itampasa mwanafunzi kujifunza kwa muda wa saa 3 tu. Mgawanyo huu wa muda unaonesha kwamba eneo la Kusoma, Kuandika na Kuhesabu linachukua 80% wakati eneo la Stadi Wezeshi linachukua 13% na Elimu ya dini 7% ya muda wote wa kujifunza. Jedwali namba 4 linaonesha muda wa kufundisha kwa kila somo.

Jedwali 4: Mgawanyo wa Muda wa Kufundisha na Idadi ya Vipindi

Somo	Idadi ya saa kwa wiki	Idadi ya vipindi kwa wiki
Kusoma	5	10
Kuandika	3	6
Kuhesabu	4	8
Kutunza Afya na Mazingira	1	2
Kuendeleza Michezo na Sanaa	1	2
Elimu ya Dini	1	2
Jumla	15	30

4.0 Rasilimali katika Utekelezaji wa Mtaala

Rasilimali za utekelezaji wa mtaala huu zimegawanyika katika makundi mawili:

- (1) Rasilimali watu, na (2) Rasilimali vitu.

4.1 Rasilimali watu: Mwalimu mahiri wa KKK

Mwalimu wa Darasa la I na la II atakuwa yule ambaye amepata mafunzo ya kufundisha ngazi hii ya elimu. Sifa za kipekee za mwalimu wa KKK zimefafanuliwa katika mwongozo wa WyEMU wa kutekeleza ujifunzaji wa stadi za KKK. Pamoja na sifa za jumla za mwalimu, mwalimu ye yeyote wa KKK anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-

a) Kufundisha

Mwalimu wa Darasa la I na la II anatakiwa kuwa na maarifa na stadi za:-

- i) Kuandaa somo linalolenga kukuza umahiri wa mwanafunzi;
- ii) Kufundisha kwa kuhusianisha stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu;
- iii) Kufundisha KKK kwa wanafunzi wenyewe uwezo tofauti katika lugha;
- iv) Kufundisha wanafunzi waliopo kwenye mwelekeo wa kushindwa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu;
- v) Kutumia TEHAMA katika kufundisha KKK;
- vi) Kutayarisha wanafunzi katika kujifunza KKK;
- vii) Mawasiliano katika kufundisha stadi za KKK; na
- viii) Kutengeneza na kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia KKK.

b) Kupima na kufanya tathmini

Mwalimu wa Darasa la I na la II awe na maarifa na stadi za:-

- i) Kuandaa zana za upimaji wa KKK;
- ii) Kutumia njia na zana zinazofaa kuwapima wanafunzi katika ujifunzaji wa KKK;
- iii) Kutunza kumbukumbu za maendeleo ya wanafunzi katika ujifunzaji wa KKK; na
- iv) Kutoa mrejesho kwa wanafunzi na wazazi ambao utaboresha ujifunzaji.

4. 2 Rasilimali Vitu

Utekelezaji wa mtaala huu unahitaji mazingira stahili ya kujifunzia na kuwepo kwa vifaa vinavyoendana na mahitaji ya mtaala. Sifa za mazingira ya ujifunzaji na vifaa ni kama vinavyooneshwa kwenye sehemu 4.2.1 na 4.2.2.

4.2.1 Sifa za Mazingira ya Ujifunzaji na Ufundishaji wa KKK

a) Viwanja vya Michezo

- i) Eneo lenye ukubwa wa kutosha linalozingatia mahitaji ya wanafunzi wote;
- ii) Eneo safi na lisilo na vitu vinavyoweza kudhuru wanafunzi wa Darasa la I na la II.

b) Darasa

- i) Ukubwa wa darasa usipungue upana mita 6.0 na urefu mita 8.0 (kwa Darasa I &II);
- ii) Ndani ya darasa wanafunzi wasizidi 45;
- iii) Dawati moja kwa wanafunzi wawili;
- iv) Nafasi ya dawati na dawati iwe mita 1.0.
- v) Kuzingatia matumizi ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu;
- vi) Kiti na meza kwa ajili ya mwalimu na msaidizi wa Darasa la I na la II;
- vii) Kabati au/na shelfu kwa ajili ya kuhifadhi vitabu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa Darasa la I na la II;
- viii) Ubao mmoja (1) wa kuandikia wenye ukubwa wa mita 1.2 upana na urefu mita 3.0 na ubao wa kutundika zana za kufundishia wenye ukubwa wa mita 1.2 upana na urefu mita 2.4;
- ix) Vibao vidogo vya kujifunzia kuandika kwenye kona tatu za chumba kwa ajili ya mazoezi ya wanafunzi.

c) Kona za Kusomea

- Kila darasa litakuwa na kona ya kusomea yenyе sifa zifutazo:-
- i) Iwe na shelfu pamoja na vitabu vya kujisomea na kadi mbalimbali za kusoma ;
 - ii) Iwe na viti, meza, benchi au mikeka.

4.2.2 Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia

Vifaa mbalimbali vitakavyosaidia utekelezaji wa mtaala vitatumika.

Wadau mbalimbali watashirikishwa katika kuandaa vifaa hivi.

a) Kivunge cha kujifunzia stadi za KKK

Darasa la I na la II watatumia kivunge chenye zana/vifaa vya kujifunzia na kufundishia stadi za KKK ambacho kimeandaliiwa kwa kuzingatia viwango vya WESTU. Kivunge kitakuwa na chati za: namba, maneno, herufi na chati za mwili wa binadamu. Vilevile kivunge kitakuwa na kadi za namba na herufi kwa idadi ilioainishwa kwa darasa husika.

b) Kitabu cha kiada na mwongozo wa mwalimu

TET kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa elimu wataandaa mwongozo wa mwalimu na kitabu cha kiada kwa kuzingatia mtaala uliopo. WESTU itathibitisha matumizi ya vitabu tajwa na miongozo. Aidha, mwongozo wa mwalimu utaenda sanjari na muhtasari wa darasa husika. Uwiano wa matumizi utazingatia mwongozo utakaotolewa na WESTU.

c) Vitabu vya ziada

Wadau mbalimbali wa elimu wataandaa vitabu vya ziada na TET itafanya tathmini kwa kuzingatia mtaala. WESTU itathibitisha matumizi ya vitabu tajwa. Aidha, WESTU itatoa orodha ya vitabu vitakavyotumika.

d) Vifaa saidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu

Vifaa vya kujifunzia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu vikiwemo vinasa sauti, visaidizi vya kusikia na Braille kwa wanafunzi wasioona na wenye uono hafifu vitatumika.

5.0 Ujifunzaji na Ufundishaji

Ipo mitazamo mingi kuhusu kujifunza kwa watoto. Mtaala huu umezingatia tafiti za karne ya 21 ambazo zinaonesha kwamba kila mtoto anaweza kujifunza kwa kuhusianisha kitu anachojifunza na maisha yake ya kila siku. Vilevile ushiriki wa mwanafunzi ndio msingi mkuu katika mchakato wa kujifunza. Katika aina hii ya kujifunza mwanafunzi anakuwa ndio kiini cha kujifunza na mwalimu anakuwa mwezeshaji badala ya yeye kuwa mtoa maarifa na mwanafunzi kuwa mpokeaji tu. Kutokana na mwelekeo huu mbinu shirikishi ndizo zitakazotumika katika utekelezaji wa mtaala huu.

Katika kufundisha kusoma mbinu ya kifoniki inasisitizwa. Mbinu hii imejikita katika utambuzi wa sauti za herufi zinaounda maneno, hivyo humsadia mwanafunzi kusoma kwa urahisi na haraka pamoja na kujua tahajia za maneno. Pia humwezesha mwanafunzi kuandika maneno kwa usahihi. Lugha zote zinazotumia mfumo wa alfabeti zina sauti nyingi zinazofanana. Kutokana na mtazamo huu mbinu ya kifoniki itamsaidia mwanafunzi kusoma lugha yoyote yenye mfumo huo kwa urahisi.

6.0 Usimamizi

Usimamizi unaofaa unasaidia katika utekelezaji wa mtaala. Wadau wote wakuu wa mtaala watashiriki katika kusimamia utekelezaji wa mtaala huu. Usimamizi utafanyika kuanzia ngazi ya shule mpaka wizara. Usimamizi katika ngazi ya shule ni nguzo kuu katika utekelezji wa mtaala. Mwalimu Mkuu, Kamati ya shule na Afisa Elimu Kata watakuwa ndio wasimamizi wakuu katika ngazi ya shule na kwa njia ya vikao watajadili maendeleo ya utekelezaji wa mtaala. Shule zitakuwa na mratibu wa KKK kwa lengo la kuhakikisha kuwa ujifunzaji wa KKK unapata msisitizo wa kutosha. Kwa ujumla usimamizi wa mtaala utafanyika kwa kuzingatia mwongozo utakaotolewa na WESTU ambao unabainisha majukumu ya wadau mbalimbali katika kusimamia utekelezaji wa mtaala.

7.0 Ufutiliaji na Tathmini

Ufutiliaji wa utekelezaji wa mtaala unalenga kukusanya taarifa kuhusu ufanisi wa mtaala. Wadau wakuu wa Elimu watahusika katika kufutilia utekelezaji wa mtaala. Wadau hao ni kama kamati za shule, walimu, wazazi, wanafunzi na wathibiti ubora wa shule. Wafutiliaji hawa wamegawanyika katika makundi mawili ambayo ni wafutiliaji wa ndani na wa nje. Walimu wakuu ni wafutiliaji wa ndani na wa mwanzo wa utekelezaji wa mtaala. Mwongozo wa ufutiliaji wa wizara inayohusika na elimu unatoa maelezo ya majukumu ya kila mdau katika kuhakikisha mtaala unatekelezwa kwa ufanisi. Taarifa za ufutiliaji zitachambuliwa na kupelekwa TET na kwa wadau wengine wakuu wa elimu ambapo zitatumika katika mikakati ya kuimarisha utekelezaji wa mtaala.

Tathmini ya mtaala ni aina ya uchunguzi unaolenga kubaini kama mtaala na utekelezaji wake unatoa matokeo yaliyokusudiwa. Tathmini huangalia mambo yote yaliyokatika mtaala yakiwemo malengo yaliyokusudiwa, maudhui, njia za kufundishia na kujifunzia, upatikanaji wa vifaa na zana za upimaji wa maendeleo ya wanafunzi, uwezo wa walimu katika kufundisha na mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Tathmini endelezi na tamati za mtaala zitafanyika kwa kuhusisha wadau mbalimbali wakiongozwa na TET. Tathmini tamati itafanyika kila baada ya miaka miwili wakati tathmini endelezi itafanyika muda wote wa ufundishaji na ujifunzaji.

8.0 Upimaji wa Ujifunzaji

Upimaji ni sehemu muhimu katika tendo la kufundisha na kujifunza. Katika mtaala huu upimaji unatarajiwu kuwasaidia wanafunzi kufanya maamuzi kuhusu utendaji wao na kupanga malengo yatakayowawezesha kujifunza zaidi. Kutakuwa na aina tatu za upimaji wa kujifunza kwa mwanafunzi.

8.1 Upimaji wa Awali

Upimaji wa awali utafanyika ili kubaini uzoefu wa mwanafunzi au mambo anayoyafahamu. Upimaji huu utafanywa mara tu mwanafunzi anapofika shulenii na utamsaidia mwalimu kutambua mahitaji binafsi ya mwanafunzi ambayo atayatumia kuandaa mipango ya kuwawezesha kufikia malengo yaliyokusudiwa. Upimaji huu pia unaweza kutumika katika kuwapanga wanafunzi, hivyo shule zinatakiwa ziwe na utaratibu wa kuwapima wanafunzi kabla ya kuanza masomo ya Darasa la I.

8.2 Upimaji Gunduzi na Majaribio Chekeche

Upimaji huu ni sehemu ya upimaji endegezo ambao unafanyika ili kupata taarifa kuhusu uwezo wa mwanafunzi katika kumudu stadi za KKK. Taarifa hizi zitumike katika kutoa ushauri na msaada unaostahili. Wakati fulani msaada wa mtaalamu wa afya unaweza kuhitajika hasa kwa watoto wenye ulemavu.

Pamoja na upimaji gunduzi, majaribio chekeche au mitihani chekeche itatumika ili kuwabaini wanafunzi wenye vikwazo katika kujifunza KKK ili kuandaa mipango ya kuwasaidia. Aina hii ya upimaji inaweza kufanyika baada ya wanafunzi kujifunza kwa miezi mitatu na kuendelea. Yapo majaribio na mitihani chekeche ambayo imeandaliiwa kutohakana na tafiti mbalimbali ambayo inaweza kutumika.

8.3 Upimaji Endegezo

Upimaji huu ni mchakato endegezo ambao unafanyika wakati wote mwalimu anapofundisha ndani na nje ya darasa. Upimaji huu utakuwa sehemu muhimu ya maandalizi ya mwalimu ambapo atatumia matokeo ya kazi walizofanya wanafunzi wakiwa ndani na nje ya darasa ili kubaini utendaji wao katika stadi za KKK. Upimaji huu utahusisha pia mitihani ya mwisho ya mihula ambayo italenga kutambua uwezo wa mwanafunzi katika stadi za KKK.

8.4 Upimaji wa Kitaifa

Kutakuwa na upimaji wa kitaifa ambapo lengo lake la jumla ni kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Hivyo Upimaji huu hautakuwa wa mchujo bali utatumika kubaini kiwango cha utendaji wa mwanafunzi kulingana na umahiri uliokusudiwa. Matokeo ya upimaji huu yatatumika kuandaa mpango wa kuwasaidia wanafunzi watakao bainika kuwa na vikwazo katika kujifunza pamoja na wale wenye mahitaji maalumu. Zana mbalimbali za upimaji zitatumika kama maswali ya kuandika, kusoma na hojaji.

Upimaji wa kitaifa utaandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania. Zana za upimaji zitasambazwa katika shule na usahihishaji utafanyika katika ngazi ya shule. Ratiba ya upimaji itakuwa moja kwa nchi nzima. Matokeo ya upimaji yatatumika katika shule husika ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji na yatawasilishwa Baraza la Mitihani la Tanzania ambalo litatoa matokeo ya nchi nzima. Ufuatiliaji wa usimamizi wa usahihishaji utafanywa na maofisa wa Baraza la Mitihani la Tanzania pamoja na maofisa kutoka maeneo mengine yanayohusika na usimamizi wa elimumsingi.

9.0 Matokeo ya Ujifunzaji na Viwango vya Upimaji

Mafanikio ya utekelezaji wa mtaala yatapimwa kwa kuangalia kiwango cha utendaji wa ujifunzaji wa mwanafunzi. Vigezo vya kupima utendaji ni kama ifuatavyo:-

9.1 Upimaji wa Shughuli / Kazi za kusoma

Mwanafunzi wa Darasa la II anatarajiwa kutenda yafuatayo:

- Kutambua sauti za herufi: Mwanafunzi wa Dasasa la II atapimwa uwezo wake katika kutamka sauti za herufi atakazopewa kwa lugha ya Kiswahili. Kiwango cha utendaji kitapatikana kwa kukokotoa asilimia ya sauti sahihi zitakazotamkwa na mwanafunzi.
- Kusoma kwa ufasaha: Mwanafunzi wa Darasa la II atapimwa uwezo wake wa kusoma kwa usahihi maneno 50 kwa dakika.
- Kusoma maneno yasiyo na maana: Mwanafunzi wa Darasa la II atapimwa uwezo wake wa kusoma kwa usahihi maneno 40 kwa dakika.
- Kusoma kwa ufahamu: Mwanafunzi wa Darasa la II atasoma habari na kutoa majibu sahihi. Kiwango cha utendaji kitapatikana kwa kukokotoa asilimia ya majibu sahihi yatakayotolewa na mwanafunzi.
- Msamiati: Mwanafunzi Darasa la II atapimwa uwezo wake wa kusoma msamiati unaolingana na ngazi ya darasa lake. Kiwango cha utendaji kitapatikana kwa kukokotoa asilimia ya msamiati utakaosomwa kwa usahihi na mwanafunzi.

9.2 Upimaji wa Shughuli / Kazi za Kuandika

Mwanafunzi wa Darasa la II anatarajiwa kutenda yafuatayo:

- Kuandika maneno na sentensi sahili kwa usahihi. Kiwango cha utendaji kitapatikana kwa kukokotoa asilimia ya majibu sahihi yatakayotolewa na mwanafuzi.
- Kutumia herufi kubwa na ndogo kwa usahihi. Kiwango cha utendaji kitapatikana kwa kukokotoa asilimia ya majibu sahihi yatakayotolewa na mwanafunzi.

- Kutumia alama za uandishi kwa usahihi (nukta, mkato, alama ya mshangao na alama ya kuuliza). Kiwango cha utendaji kitapatikana kwa kukokotoa asilimia ya majibu sahihi yatakayotolewa na mwanafunzi.
- Kuandika hadithi fupi/aya yenyeye ushikamani, tahajia, muundo wa sentensi, na vituo sahihi. Kiwango cha utendaji kitapatikana kwa kukokotoa asilimia ya majibu sahihi yatakayotolewa na mwanafunzi.

9.3 Upimaji wa Shughuli / Kazi za Kuhesabu

Mwanafunzi wa Darasa la II anatarajiwu kutenda yafuatayo:

- Kujumlisha na kutoa: Kufanya matendo ya kujumlisha na kutoa kwa namba zenyeye tarakimu tatu. Kiwango cha utendaji kitapatikana kwa kukokotoa asilimia ya majibu sahihi yatakayotolewana mwanafunzi.
- Kukamilisha mtiririko wa namba: Kujaza namba moja inayokosekana kwenye mtiririko wa namba nne. Kiwango cha utendaji kitapatikana kwa kukokotoa asilimia ya majibu sahihi yatakayotolewa na mwanafunzi.
- Sehemu: Kutambua na kuhusianisha michoro inayoonesha sehemu za michoro na sehemu za numerali. Kiwango cha utendaji kitapatikana kwa kukokotoa asilimia ya majibu sahihi yatakayotolewa na mwanafunzi.
- Maumbo: Kutambua, kubaini na kuchora maumbo rahisi na mistari. Kiwango cha utendaji kitapatikana kwa kukokotoa asilimia ya majibu sahihi yatakayotolewa na mwanafunzi.
- Vipimo: Kutumia vipimio rahisi ambavyo ni rasmi na visivyo rasmi kutambua muda, ujazo, uzito na urefu. Kiwango cha utendaji kitapatikana kwa kukokotoa asilimia ya majibu sahihi yatakayotolewa na mwanafunzi.
- Data: Kutafsiri data rahisi zinazoelezea vitu au shughuli. Kiwango cha utendaji kitapatikana kwa kukokotoa asilimia ya majibu sahihi yatakayotolewa na mwanafunzi.